Title: VALLEY OF WEEPING
Preached by Dr. w euGENE SCOTT, PhD., Stanford University
At the Los Angeles University Cathedral
Copyright © 2007, Pastor Melissa Scott. - all rights reserved

Somo: BONDE LA KILIO
Imehubiriwa na Dk. w. euGENE SCOTT, Daktari wa Falsafa, Chuo Kikuu cha Stanford
Katika Kanisa Kuu la Chuo Kikuu cha Los Angeles
Haki © 2007, Mjungaji Melissa Scott. – Haki zote zimehifadhiwa

# BONDE LA KILIO

Kama unanyofahamu, kuna jumbe saba ninazohubiri kila mwaka ukijumuisha na ule ujumbe wa Pasaka. Nilihubiri siku ile ya msiba wa baba yangu, kwa hiyo nitaacha ule ujumbe wa kawaida wa Pasaka na nihubiri moja kati ya zile jumbe saba ninazozitazama kila mwaka. Ujumbe huu umekuwa mwanga wangu wa kiroho ukiniongoza katika miaka yangu ya utu uzima na katika kipindi chote cha huduma yangu—Zaburi 84: “Heri ambaye nguvu zake zatoka kwake.”

Pigia mstari neno“heri”. Sasa makanisa yanajihusisha na baraka ambazo ziko kwa muda na mahali, lakini neno ka kiebrania hapa linaelezea hali ya kubarikiwa ambayo haibadiliki.

Sasa nimehubiri katika ujumbe huu—mstari huu, kwa muda wa zaidi ya miaka 30. Sijui jinsi ya kuelezea tofauti na nilivyohubiri. Tatizo ni kwamba ninahitaji kuhubiri tena kila mwaka kwa sababu sijafika hapo bado. Najua kwamba Waebrania wanachosema. Inaelezea hali ya baraka ambazo hazibadiliki. Sio kitu cha muda tu. Ni “kitu cha ziku zote” hali ya kubarikiwa. Sijafika huko bado, lakini najua jinsi ya kufika hapo. Ndio maana nahubiri ujumbe huu. Ni hali ya baraka ambayo sio kila mmoja anapata—“Heri yule ambaye.” Makala inamtenga huyu mtu kutoka kwenye kundi. Si kitu, ni pumzi iliyotoka mbinguni. Ni aina ya mtu ambaye ambaye ana hii baraka. “Heri ambaye nguvu zake zatoka kwake; na njia ziendazo Sayuni zimo moyoni mwake.”

Mstari wa 6: “Wakipita”—hiki kitendo kinafanya wazi baraka zilizo kwa mtu fulani ambaye anaelekea sehemu fulani, ni mchakato wa mabadiliko. Sipendi baadhi ya vipengele. Ninazeeka sasa na inafanya nisipende mabadiliko, nimeshapitia mambo mengi sana na hakuna kitu chochote zaidi Mungu anachohitaji kunifundisha, husunani mambo ya aina hii.

Nilipokuwa na umri wa 30, nilizoe kuhubiri hivyo. Ningekuwa ndani ya kanisa lenye watu wenye mvi na ningeweza kuhubiri kwa nguvu. Hebu elewa hili kuhusu ukristo—hakuna kukaa mahali pamoja. Hakuna kufuzu, hakuna kufikia malengo, hakuna wakati utakaofika utulie na useme, “Tazama hawa viumbe wote walioko kwenye taabu wanajaribu kufikia hapa nilipo.” Ukristo ni safari, sio hatma—mpaka tutakapofika hapo mwisho. Hii ina maana kuna mabadiliko ndani yake.

Agano la Kale linasema kuhusu taifa ambalo Mungu hakulifikiria sana, anasema “walitulia kwenye kibanda.” Ni neno linalotokana na watengenezao mvinyo; ina maana “walitulia”. Na anaendelea na kusema hawakutolewa kutoka kwenye chombo kwenda kwenye chombo; ”kwenye hicho kibanda chao” bado liko ndani yao walinuka na kutoa harufu mbaya kwa sababu walikuwa bado hawajatolewa. Mchakato wa kutengeneza mvinyo ungesafisha chombo kimoja kwenda kingene na ungeacha kibanda nyuma.

Nilipokuwa mtoto nilizoea kulala hapo. Lazima utegemee mabadiliko. Ushindi wa leo unakuweka kwenye mashambulizi ya Shetani. Na hakuna mahali katika hii safari ya Ukristo unayoweza kukata tamaa na kusema, "mmmh! Ninachotakiwa kufanya sasa nimeshaweka alama ya ukumbusho na nimeshafikia alama zangu na nimehakikisha kuwa niko vizuri na Mungu, ninapumzika hapa na nasubiri Mungu anachukue kwenda nyumbani." Mmmh! Sasa kama hupendi hili, hautakuwa karibu nami.

Nilizoe kuhubiri kupitia hii sehemu ya ujumbe upesi sana kwa sababu ilikuwa inaeleweka. Nilipokuwa kijana na nikiwa naenda mahali fulani. Sasa hii ni sehemu ya jumbe ninazozichukia. Lazima utakuwa usikiliza kwa miaka kumi na mitano, nilizoe kupitia hii sehemu upesi sana. Ningemnukuu Dk. Tozer: "Ukristo ni safari, sio hatma." Ningeonyesha makusudi mengi ya Ukristo kwa ajili ya kufikia kusudi kubwa moja: ningeshuka chini ya madhabahu, ningesema baadhi ya hotuba za siku zote; uko salama, ningewapiga kibao kidogo mgongoni, na kuwatoa nje. Huu ndio—ulinzi wa milele! "Fanya chochote upendacho! Umeshafanikiwa! Umeshalipa muda kwenye bima yako—uko ndani sasa! Sasa unatoka hapa mpaka nikifanya nafasi kwa ajili ya mwingine. Wewe ni kiganja kwenye mkanda wangu!"

Wapentekoste walienda mbele zaidi, na kazi ya pili ya neema, watu walienda mbele zaidi, na walikuwa na uzoefu wa pili ambao watu wanao; na ukishawapata, unawapungia wote waliobaki ili wakupate; na ukishawapata, unakuwa zaidi ya wengine na hutakuwa na kingine zaidi cha kutafuta. Nimekuambia nipokuwa kijana katika misingi ya kanisa la kipentekoste, tulikuwa tukienda kwenye mikutano kambini kwa sababu watoto wengine wote walikuwa navyo, na tulipokuwa nje tukicheza mpira; na walikuwa wakijaribu kunipa mimi ule mmea kwenye vumbi ndani ya hema. Sikumhitaji Mungu sana, ili kumaliza hilo tulicheza mpira.

Hatma! Kama Reinhold Niebuhr alivyosema, balaa la uzoefu wa Kipentekoste na kazi ya pili ya watu wa neema—Wanazareno, na wao walielewa kuna uzoefu zaidi ya mwanzo, ni ule uzoefu ulioleta hali ya juu ya kutotenda dhambi ambao umekuwa chombo cha dhambi iliyo mbaya sana: kiburi cha kiroho. Wakiweka kambi hapa na walimpungia kila mmoja wao.

Hakuna mwanzo. Ndio maana ndio kwanza tunaanza huduma mpya: kila kitu kimeshaandaliwa;mafunzo yameshatolewa; kila kitu kiko tayari kuifanya dunia jumuiya yetu. Kweli, kama tukichukua hatua mpya ya imani, tunatambua kwamba sisi ni mahujaji hapa. Tuko safarini, na huu mstari, sambamba na hiyo kweli, anasema huyo mtu aliyebarikiwa, huyo mtu aliyetengwa na kundi la watu, ambaye ana hali ya kubarikiwa katika maisha yake ambayo kamwe haitamwacha, yuko safarini— siku zote ikibadilika.

Kifungu cha pili kinasema, "Yeye anayepita kwenye bonde la Baca". Unajua baca ina maana gani? Ngoja nisikie kutoka kwako! Baca ina tafsiri ya "kilio". Sasa ni mbaya zaidi kuliko nilivyosema—sio mabadiliko ya siku zote, maisha ni yale ya mtu fulani katika safari ya mabadiliko na katika safari hiyo … (na nawakumbusha hii Pasaka ya mwaka 1991, tunavyotazamia mwaka mwingine), sehemu ya safari kupitia mtu aliyebarikiwa anapokwenda ni "bonde la vilio". Hivyo kila wakati tunaruhusu fikra ziingie kwenye Ukristo kwamba kama uko vizuri na mapenzi ya Mungu, hautakuwa na mabonde la vilio.

Biblia yangu inasema mtu aliyebarikiwa, wakati katika hali ya kubarikiwa—hakuna sifa za kwamba hali ya kubarikiwa inabadilika, nenda kwenye mabonde la vilio.

Niko pale nilipokuwa Jumapili iliyopita nilipohubiri kutoka kitabu cha Isaya, "Ni nani miongoni mwenu amchaye Bwana, yeye aendaye katika giza, wala hana nuru?" Nimeshachoka na hii dini ambayo inaunda vitu, narudia, fikra ambazo unajikuta moja kwa moja uko kati kati ya bonde la vilio, ina maana una mtu ambaye amemuacha Mungu au Mungu amemuacha yeye. Ni moja ya safari! Kuanzia kati kati ya wiki hii nzima nahubiri au kufundisha Kutoka, kongamano la Agano la Kale ambalo Mungu aliwaongoza jangwani… Kumbukumbu la Torati linasema, "kuwajaribu na kuona yaliyo moyoni

mwao”. Na wiki iliyopita tumewatembeza kutoka kwenye ushindi wa bahari ya Sham ambapo Mungu alifanya kila kitu. Walichofanya ni, “Simameni na muuone utukufu wa Bwana.”

Kutoka kwenye ushindi wa bahari ya Sham ambapo hawakufanya kitu chochote…. (Unajua, siwezi kukumbuka ni lini Mungu amekuwa mwema kwangu.) “Simameni”, Musa alisema, “na uuone wokovu wa Bwana.” Aliigawanya bahari ya Sham na kuuwa adui wake wote. Na umenisikia mimi kwenye vita vya Ghuba. Unajua, nasikia hawa wakristo huwa wanawaombea adui zao. Mimi siwaombei. Ninawaombea ili wawe wafu zaidi ya kupigika, na nina Biblia nzuri sana. Nina maana watakatifu wote wa Agano la Kale walisimama kando ya bahari ya Sham baada ya jeshi la Farao kuzama kama jiwe. Mungu ni mwema. Aliondoa magurudumu kutoka kwenye gari kabla ya kubadilisha maji; walikuwa wakienda mbele na kurudi nyuma na wakazama.

Na watu wa Mungu walicheza na kushangilia: “Angalieni mambo ambayo Mungu amefanya kwa ajili yetu! Alimzamisha Farao wa zamani kwenye bahari ya Sham kama jiwe.” Kisha Mungu aliwatembeza jangwani kwa siku tatu ambapo walikuwa na kiu na wakinung’unika, kwenye maji ya Mara ambayo yalikuwa machungu. Walikwenda kutoka jangwa la Shuri kwenda kwenye sehemu nyingine ya baraka, Elimu yenye visima kumi na viwili na minazi 70. Ukifikiria kuhusu hili, haikuwa jua kali kwao kwa sababu walikuwa watu millioni tatu na laki mbili na nusu kupigania visima kumi na viwili na minazi 70. Lakini kisha, aliwaongoza kuelekea kwenye jangwa la “dhambi” lililotafsiriwa kama “udongo” ambapo aliwalisha manna kutoka mbinguni na kuwafundisha kwamba yeye ndiye mpaji wao siku hata siku.

Kisha wakaenda kwenye mlima Sinai ambao una maana ya “Mungu wa dhambi” ambayo “Sehemu ya udongo ya Mungu” ambapo walijifunza masomo. Kwa kifupi, lilikuwa ni jangwani ambapo walijifunza ushindi wa Mungu na walijifunza uwezo wake wa kutoa. Hawakujifunza zaidi kushangilia kando ya bahari walipouona mkono wa Mungu wenye ushindi; hawakujifunza sana katika visima vya Elimu; hawakujifunza sana kwenye mlima Sinai wakati Mungu alipokuwa akioengea na mlima—walikuwa wakicheza karibu na ng’ombe wa dhahabu na wakafanya sherehe.

Ni wakati wa kujaribiwa kwa wakristo uliwachambua wale walionacho na wasionacho. Na hili ndilo “bonde la vilio” kama vile “jangwa la dhambi”, au tukiwafuata wiki ijayo waliongozwa kwenye sehemu inayoitwa Refidimu ambayo ina maana ya “sehemu ya mapumziko”, na ilikuwa ngumu, chafu na yenye miamba…. Njia za Mungu si kama njia zetu. Ninachotaka kupitia, na kisha nitakiacha, ni kile ambacho kiko kinyume na mahubiri ambayo yanaufanya ukristo ushindane na baadhi ya vitu vinavyoleta ushindi na maisha mazuri upesi upesi, kwa hiyo mtu aliyebarikiwa maandiko yanaonyesha njia yake inaenda kupitia mabonde ya vilio.

Nimejikumbusha mwenyewe kuhusu jambo hilo mwaka uliopita. Vilio viko tofauti sio kama vilivyokuwa mwanzo. Ninaweza kukumbuka aina ya mabonde niyopitia nilipohubiri hili somo kama mmisionari nilitembea duniani kwa miaka 18. Sasa mabonde ya vilio yanaonekana kuwa ya tofauti. Kuna nyakati natamani hili kanisa kuu lisingekuwako. Kuna nyakati uzito na mgangamizo wa baraka za Mungu ambazo zimetufanya tuwe zaidi ya zile baraka ambazo Mungu ametupa kutusaidia ili kazi isonge mbele, na kama sio uwezo unaozidi nguvu zao wenyewe na nguvu zangu—mabonde yanachukua nafasi ya tofauti.

Lakini bado kuna ukweli kuwa uzoefu wa kikristo kama unasogea mbele ukimfuata Mungu, watu hawa wanokaa kwenye runinga na wakikuangalia huku wakitabasamu na waenenda kama vile aidha hakuna dalili yoyote ya wingu angani ambayo ni uongo au hawamjui Mungu. Wanamtumikia mfalme wa ulimwengu huu. Na kwa sababu Mungu sio dhalimu, anajitahidi kuwasukuma watu hao taratibu. Ni wale walio wa Mungu lakini Shetani anaendelea kuwakamata.

Bado sijakwepa mabonde ya vilio. Sizungumzii kuhusu hayo majanga ya asili—nimekuwa nikilia na kumkumbuka baba yangu mara nyingi. Naongelea kuhusu mabonde ya kiroho pale inapoonekana umechukua hatua za kiroho na Mungu haja…. Kuna kitu kimoja kuhusu Mungu ambacho hakiyumbi ni kwamba: Anaenda sehemu yoyote, kila wakati mara tu baada ya kunihamasisha nifanye jambo fulani kwa ajili yake.

Umeshagundua hicho? Nimeshaanza kuchoka kuhusu mambo ya Mungu na kusema, "Oh!"— ninaongea wazi na Mungu—"Elewa hivyo! Jambo lingine baya nililonalo! Umenipata. Umenipata. Kwaheri"—na hataniacha peke yangu.

"Nimekuja kwenye amani! Ninaachana! Mungu anayo"—na atachukua kitambaa changu cha mkononi na kunifuata na kunisumbua njia nzima—kila wakati! Hashindwi kamwe, kwa hakika anatanitosheleza. Nitasema, "vema, kuna kitu fulani cha imani kwenye hii njia hii ya imani! Nitaiendea hiyo njia. Sote kwa pamoja twende kwa Mungu!" Kisha anakwenda likizo kila mara— kila mara! Usione hivyo kama ni kushindwa. Hizo ni aina za mabonde ya vilio ninayoyazungumzia. "Uko wapi Mungu? Ni uchafu mwingine tena umenipata!"

Hakuna kitu kingine tena…, nimeshasema, Mungu anaweza kunifundisha. Ninajua ninachohubiri leo—kwa nini ninatakiwa kuendelea kujifunza kila mwaka? Unafikiri kila kitu kiko kwenye chuma, bila kutegemea kinakuja kitu ambacho kinazima kila kitu . Kama vile askari mzee ambaye amekuwa vitani mara nyingi, siamki kirahisi siku hizi tena. Ilikuwa vita vikubwa nilipoanza kama mkristo. Sikujua kama shetani ni mgumu kama alivyo. Ningeweza kuimba nyimbo za kipumbavu kama vile "andika jina la shetani chini ya kiatu chako na kitembelee ukimkanyaga." Nina maana zile tatuu za kininja, nitakwambia hivyo!

Nilijua ahadi zote za Mungu, na ningewasikiliza wahubiri na bado ningeweza kukuambia, ningewaona wote wakitoa macho: "Shetani yuko chini ya miguu yako! Shetani yuko chini yako na Mungu emekwisha mshinda 'yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia'!" Na ningesema "Ni vema!" na kisha Shetani angenigonga hatua 75. Ningesimama na kusema, "Hivi vita ndio kwanza vinaanza!"

Sasa ningetembea kwenye miti kumkwepa Shetani. Nimechoka kupigana; nimechoka na vita. Sitaki tena mabonde ya vilio. Nimewambia Mungu mwaka mzima, na akasema, "mimi ni bosi! Mabonde ni sehemu ya safari." Sitaki ushangae mwaka huu. Shangilia, watakatifu! Itakuwa mbaya zaidi. Nitakwambia kitu fulani, Shetani akiwa …. Mwishoni ninapokuwa nikiamka, akaridhika zaidi!

Sasa kanisa halitanyamaza kimya. Na sitarajii kustaafu, ninafahamu sana uwezo wa Shetani na silaha zake. Na ninaweza kusema kuwa mhubiri alisema bila kuwa na nguvu: "yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Na sasa najua, ingawa nimejifunza tena kutoa Biblia na kufanya ninachofanya leo tunavyoingia mwaka huu; na ninategemea kutangaza Siri Tano zimekuwa kweli. Na tunavyovamia eneo la "mwana wa mfalme wa anga" na kufanya tunanyoweza kufanya. (Hii ni redio kubwa na yenye nguvu iliyowahi kuwepo duniani). Ninategemea Shetani ataondoka kwa sababu anajua tunavamia eneo lake. Na ninataka awe tayari— kwa kanisa …, kwangu mwenyewe…, na ninatakwa uwe tayari kwa mabonde ya vilio yatakayokuja. Na nitataka uweze kuyafanyia kazi wewe binafsi—mabonde ya vilio ni sehemu ya safari. Hautakiwi kukata tama kwa sababu mabonde yako pale.

Nitasema mambo mawili ninayosema mara kwa mara ninapohubiri ujumbe huu. "Chanzo" sio muhimu. Ni njia ya Shetani tu unapoingia kwenye mabonde kuanza kujishughulisha na "kwa nini". Kama umefanya makosa na utajilaumu, unajua hivyo, Shetani anapenda kukupiga na kukuua ukiwa na ufahamu wako. Atakaa kwenye bega lako moja na atasema, "Vema, uwe mtu yule. Unamlaumu—

unajua ulichofanya; umevumilia" Vema ninataka umwambia Shetani katika jina la Yesu anapokufanyia jambo baya, "Toka! Toka!"

Unaweza kuuchukua mstari huu wa maandiko na kuiwekea alama hiyo sentensi. Hakuna lolote katika huu mstari kuhusu "chanzo". Haijalishi kama utakuwa wa kulaumiwa au hapana. "Amebarikiwa", na hili ni neno linalofuatia ninalitaka ulipigie mstari, "kupitia katika mabonde ya vilio". Unaweza ukajiweka mwenyewe kwenye kifo kwa fikra zako—weka kambi na jenga nyumba ndani yake. Hakuna neno kwenye mstari huu kuhusu "chanzo" ni sentensi tu inayosema "waliobarikiwa wanapitia."

Kama ukiwa unalaumiwa kwa kukosea kwako, liweke hilo jambo msalabani. Kristo alikufa ili aweze kuzifunika dhambi zetu. Unatakiwa kuwa muwazi mbele za Mungu kuhusu hilo jambo. Haijalishi kwako kama uko kwenye bonde lako "kukosea/kuharibu", ujumbe wangu kwako leo ni: "watu waliobarikiwa wanapitia!" Haijalishi ni chanzo gani. Acha kujilaumu mwenyewe. Huawezi kuibadilisha historia. Huu ndio uzuri wa neema ya Mungu. Mwachie yeye. "Vema, siko hapa kujilauma!"

Au ni kinyume; "Hakuna sababu kwa kile kinachonitokea. Nimekuwa mwaminifu! Nimefanya nililoweza kufanya na dunia nzima ilinitupia mimi." Shetani ataruka kutoka kwenye bega la ushitaki kwenda kwenye bega la kuhurumia. Anapenda kufanya hivyo! "vivyo hivyo ni sawa. Nisingemtumikia Mungu anayefanya hivyo au anayruhusu hayo yatokee kwako. Sio wa kulaumiwa kwa kitu chochote." Hayo mambo yanapotokea, unasema "shauri yako!" haijalishi kitu. Haijalishi kama wewe huna hatia. Mabonde ya vilio ni sehemu ya safari, lakini watu waliobarikiwa wanapitia. Itakuwa huruma, "Huruma, kukata tamaa, aibu juu yangu". Acha kurudi nyuma katika bonde lako.

Ninahubiri dini iliyokuwa! Mabonde ya vilio ni sehemu ya safari. "Mvua inawanyeshea sawa sawa wote walio na haki na wasio na haki," lakini wamebarikiwa watu wale wapitao kwenye hayo mabonde. Njoja niongezee kitu kimoja; hawapitii tu kwenye hayo mabonde, hakuna kitu chochote kwenye mstari huu kinachoelezea ni urefu gani hayo mabonde yanao. Unaweza kuvuka hatua moja ndefu au unaweza kuwa ndani ya hiyo hatua kwa muda mrefu. Mstari hausemi: "wamebarikiwa watu wale wapitao kwenye mabonde wasiofikiri mabonde yatawaua," ni uhakika wa ahadi za Mungu: "utafanikiwa," Hii sio dini ya kufikirika ambayo inasema kilicho kweli si kweli. Mabonde yako ni mabaya kama vile unavyofikiri, lakini haijalishi kama ni wa kulaumiwa au huna hatia—"Wamebarikiwa wanaopita."

"Ninatoka nje; leo ingeweza kuwa ni ile siku!"—usijaribu kuabadilisha hiyo tabia! "Wamebarikiwa wanaopitia!"

Katika muda mwingi wa maisha yangu inakuwa nafuu… Niyachambue leo, kidogo ingenifanya niwe kichaa, lazima nikiri hivyo, lakini inakuwa nafuu zaidi. Ilikuwa hivyo, maisha yangu yalikuwa na bonde moja refu lenye matuta ya mara moja moja…. Ni mbaya sana! Haiwezekani! Huwezi ukawa kwa watu hawa kwenye misemo ya kiroho! Sasa kwa nini nasema inakuwa nafuu? Tuendelee.

Sio tu wale waliobarikiwa ndio wanapitia "Amebarikiwa mtu yule anayepitia kwenye bonde la Baca"—au "kilio", "na kulifanya kisima". Chanzo kinasema: wamelifanya kuwa "sehemu ya chemchemi". Sijui kama unafahamu kwamba tungeweza kukaa katika bonde la mtaa wa matumaini? Kama kawaida, mabonde mabaya yanakuwa kwa wale walio wapendwa, wakristo. Lakini tumefanya hayo kuwa "sehemu ya chemchemi" kwa sababu hatusemi "Hapana".

Hatuwezi matukio kama jibu la mwisho. Waliobarikiwa hawafi kwenye mabonde yao. Hakika, lengo la mtu aliyebarikiwa katika mstari huu sio kudumu daima—aina hii ya mtu hubadilisha mabonde. Huyaona mabonde kama chanzo cha kuleta 'sehemu ya chemchemi.' Kuna nyakati chache…. Nilikuwa nazo

nilipokuwa nikisafiri sana—kuna muda angalau usiku mmoja wakati wa kampeni au hata jioni moja ningeenda na mchungaji hospitali.

Nimekuwa na uzoefu kule nilikokuwa nikiwatembelea watu kando kando na nikitoka nikiwa nimebarikiwa nao. Unabadilisha hilo bonde ambalo lingeweza kuwaponda watu wengine—na hii ni alama ya ukristo, unaenda kwenye "sehemu ya chemchemi" mpaka vile bonde linakuwa chanzo cha kuleta baraka zaidi.

Sasa swali ni kwamba, kwa jinsi gani waliobarikiwa wanapitia kwenye mabonde ya vilio—wanapitia kwenye hayo mabonde; wanayafanya kuwa mahali pa chemchemi. Kwa vipi? Nenda kwenye mstari wa kwanza, "Amebarikiwa mtu yule ambaye nguvu zake"… Unasemaje huu mstari? "nguvu zake zi ndani ya Mungu." Huu ni uthibitisho! "Amebarikiwa mtu yule ambaye nguvu zake zi ndani ya Mungu." Yesu hakusema kuwa tutapitia kwenye mabonde. Ni kweli alisema duniani kuna dhiki. Alisema atakuwa nasi katika hayo mabonde—hatatuacha. Yesu si Mungu wa vilele vya milima tu. Ahadi ya Mungu ni kwamba sisi tutakaposimama kwenye imani na kuweka mkono wetu kwake, hatatuacha.

Huo ndio ulikuwa ujumbe wa Jumapili iliyopita: "Usitie shaka katika giza kile ulichojifunza kwenye nuru." Unaweza usimuone Mungu; lakini yeye anakuona. Hakika,"wale Mungu awapendao huwafundisha." Hiyo ni Waebrania. Hakika Petro anasema, "Kuna dhiki nyingi", na anatumia lile lile neno la kigiriki "baraka nyingi". "Mungu hatujaribu zaidi ya tunavyoweza kukabiliana na jaribu, lakini katika kila jaribu ataonyesha njia ya kutokea"—na kwa mgiriki ana njia ya kutokea na iko kwa mtu binafsi kama vile jaribu lilivyo, kama nilivyosema Jumapili iliyopota. "Amebarikiwa mtu yule ambaye nguvu zake ziko kwake."

Mungu alimwita Eliya—akamtuma kwenye kijito cha Kerithi; akawaamuru kunguru wamlishe, lakini Biblia inasema baada ya muda kijito kilikauka. F. B. Meyer alisema Mungu alikuwa akimfundisha Eliya kumtumaini yeye mtoa vipawa badala ya vipawa ambavyo yeye anavitoa. Mungu anavitwaa vitu vyote tulivyonavyo, kama nilivyosema pale mwanzo, kutoka chombo kwenda chombo. Haya mabonde ya vilio yamewekwa kutufundisha kumtegemea Bwana. Yeye yuko pamoja nasi na kama nguvu zake ziko pamoja naye, kisha ninachojua ni kwamba ninatembea na Mungu na mabonde hayajalishi kitu. "Amebarikiwa yule ambaye nguvu zake ziko ndani yake, ambaye moyo wake uko ndani yake." Ni wangapi wameandika kwenye Biblia zao kwa kutumia maneno ya kitalino? Hebu ngoja niione mikono yako. Maneno ya kitaliano yana maana: yamejumuishwa kwenye tafsiri. Maandiko ya mwanzo yanamaanisha "yeye". "Amebarikiwa mtu yule ambaye nguvu zake ziko ndani yake, na ambaye moyo wake uko katika njia zake." Jitahidi—imeelezwa na mtasfiri. "Kila kitu kiko katika njia zake."

Mungu sio kwamba anatupenda tu, ni kwamba anatulinda na anatupitisha pia kwenye mabonde na anataka tuzijue njia zake. Tutatawala na kumiliki milele yote pamoja naye, na ataka tuzijue njia zake. Baada ya miaka arobaini jangwani, Mungu alilalamika kwamba wana wa Israeli waliyaona matendo yake tu; Ni Musa pekee alizijua njia zake. Ni nani kati yenu anayeweza kushuhudia kwamba kwa kipindi chote hiki cha miaka kumi na mitano amezijua njia za Mungu? Zaidi na zaidi unamwona yeye.

Vema, hebu ngoja nimjaribu mmoja kati yenu. Ni wangapi kati yenu mmejifunza kwamba Mungu anatarajia mambo mengi kutoka kwako, yeye alifanya ulivyoanza? Vema, unajifunza njia za Mungu. Ni wangapi wanaogundua kwamba sio rahisi kwa Mungu kulazimisha shuhuda za kuonyesha jinsi unavyojitoa kwake? Unajifunza njia zake. Anakupeleka nyumbani, anakulinda. Mtu ambaye chanzo cha nguvu zake ziko kwenye ufahamu wa Mungu mwenyewe, na uwepo wake kwako, na njia za Mungu, yeye haanguki kwenye mabonde ya vilio.

Sasa ninamaliza. Mstari wa 11: “Kwa kuwa Bwana Mungu ni jua na ngao.” Hii ni sehemu ya njia zake; “Bwana Mungu ni jua na ngao.” Hiki ndicho anachojaribu kutufundisha. Kazi ya jua ni nini katika ulimwengu huu? Kila kitu kinalizunguka, linatawala njia za vitu vingine kwanye sayari. Mtu mmoja mpumbavu alifikiri kwamba jua linavizunguka hivi vitu. Jua linatawala; jua linaleta uhai, linatoa joto joto. Pasipo hilo tusingekuwa marafiki wazuri. Hicho ndicho mtu yule aliyebarikiwa alikuja kukijua: Bwana ni yote katika yote.

Nitasema hivi: siyapendi sana mabonde, lakini niko kidogo …. Bado naongea na Mungu kuhusu mambo mengi, lakini si sana. Ninaamini nina ulinzi mkubwa wa Mungu kuliko hata Mchungaji wako alivyokuwa alipokuja hapa miaka kumi na mitano iliyopita. Nina hakika ninataka kuwa. Ndicho tunachojifunza tukiendelea. Siyapendi mabonde ninapokuwa ndani yake, lakini yamenifundisha mambo mengi ambayo ushindi haukunifundisha. Na wakristo wanajifunza kumtegemea Mungu na kumfanya “mwana” atawale.

Ngao. Hii ni sehemu ngumu kwangu mimi kuikubali: kuamini kwamba Mungu haruhusu jambo lolote kutokea ambalo haliko kwenye mpango wake. Kama Bwana wa Majeshi alivyo, Shetani yuko chini yake. Mapepo bado yanatikisika katika uwepo wake, kama vile Mungu anavyoinua ile ngao juu ya Ayubu, kila kitu kilichotoke kwako mwaka uliopita, kila kitu kitakachotokea, kila bonde la kilio litakalokugonga, Mungu ambaye ni ngao yako—katika hekima yake hutufundisha, anaruhusu mambo hayo yatokee. Uwezo wake kukabiliana na mabonde ya vilio haupimiki zaidi ni pale unapoamini kwamba uko katika ulinzi wa Bwana; yeye kama ngao hataruhusu jambo lolote litokee ambalo huwezi kulikabili.

Namba 3. “Bwana atakupa neema na utukufu.” Kweli, mabonde yanakuja na yanaleta kibali kisichostahili. Nimeshasikia. Nimekuwa nikchukizwa na haya ninapokuwa nikitazama kanisa la kidunia, baadhi ya wahubiri wanapokuwa katikati ya mimbari wakiwa wamejivika utukufu wote na wanapenda kusema ule msemo wa kitheolojia, “Mungu hatamshirikisha mtu yeyeto utukufu wake” wanaposimama pale na kusema ambacho Mungu hawezi kufanya. Biblia hapa inasema Mungu ataonyesha utukufu. “Mungu anatoa neema”—neema tusiostahili, “na utukufu”. Kitu ambacho Mungu hataweza kushirikiana na mtu ni utukufu. Lakini atautoa utukufu wake—atabariki; atakuvika heshima. Kuna mabonde ya vilio, lakini hiyo siyo safari yote—unayapitia, na Mungu anakupa neema; na Bwana anakupa neema; na Bwana anakupa utukufu.

Kabla ya kufika mwisho, ninataka tuangalie mstari wa 8: “Ee Bwana wa majeshi.” Ni kweli unajua jina hili lina maana gani? Nilihubiri kuhusu majina ya Bwana Jumapili iliyopita. Hili ndilo linaloongelea kuhusu uwezo wake kudhibiti kila kitu. Nimekwishasema kuhusu Shetani na mapepo yake, Mungu atam…. Kuna nyakati katika Biblia, vita vya Debora na Baraki, ambapo Mungu alizishirikisha nyota zikajiunga kwenye vita. Alilimeza jeshi la Farao kwenye bahari ya Sham. Kama Bwana wa majeshi, anadhibiti hata vitu visivyo na uhai. Anadhibiti ulimwengu. Anadhibiti vitu vyenye nguvu nyingi, malaika na mapepo wote. Anadhiiti nchi na mataifa, na anayafanya kwa nyakati zake.

Hiyo ndio maana ya jina lake “Bwana wa majeshi”. Ina maana tatizo lolote mimi na wewe tunalokabiliana nalo, anaweza kutatua. “Ee Bwana wa majeshi, Bwana wa majeshi, sikia ombi langu: nitegee sikio, Ee Mungu wa Yakobo. Au “fikiria hilo”.

Sasa unaweza kusoma ule mstari wa 8 na usipate kitu chochote kama ukiwa na haraka, kwa wakati ule ile Zaburi ilipokuwa imeandikwa, Yakobo alikuwa ameshakufa. Yakobo alikuwa amegombana na malaika usiku mzima, Yakobo—jina lake lina maana ya “aliyekamata kisigino”, kila mara anakamata na kutafuta kwa ajili yake mwenyewe—ujanja, Yakobo mbinafsi jina lake lilibadilishwa na Mungu kuwa “Israeli” likiwa na maana ya “mwana wa mfalme ambaye ana nguvu za Mungu”. Katika huu mstari,

Mungu kwa kupitia mtunga Zaburi anasema kitu fulani muhimu sana kwetu sisi tulio bado kwenye mabonde ya vilio; ambao kila mwaka tunajifunza kumtumainia Bwana pekee; na kujifunza njia zake, ambao wanamlilia Mungu alete nguvu zake kukabili matatizo yake. Bwana wa majeshi yeye ndiye jina lake.

Nina maana ulikuwa ukiongelea tatizo dogo la kifedha au ugonjwa, au binti yangu au kijana wangu au mtu ninayempenda katika Ghuba, na tunalia "Bwana wa majeshi, katika bonde la kilio—wewe unayepanga kila kitu ambacho kipo na unaweza kujishughulisha na tatizo langu dogo? Haisemi, "Ee Bwana wa Majeshi, lisikie ombi langu: nitegee sikio lako, Ee Mungu wa Israeli." Kama ingesemwa, "Ee Mungu wa Israeli"—na ninarudia, Yakobo alibadilisha asili yake na akabadilisha jina lake. Alikufa kama "Israeli" sio "Yakobo". Kama ilisemwa, "Tega sikio lako, Ee Bwana wa Majeshi, Ee Bwana wa Majeshi," Ningesema, "Vema, ninatakiwa kufanya mabadiliko makubwa kabla Mungu hajanisikiliza!" Lakini inasema, "Ee Bwana wa Majeshi, sikia ombi langu: Ee Mungu wa Yakobo"—huo ni ujanja, kukamata mnyoo unaoitwa Yakoko alipotoka kwenye tumbo la mama yake kwa sababu ya njia zake za kibinafsi.

Ni kipi Mungu anachotaka kusema kwao, wewe na mimi, ambao tunapambana na tunaenda kupambana na mabonde ya vilio? "Yupo: Bwana wa majeshi, Waitikiaji: Mtu yeyote kati yetu—kwa sababu Bwana wa majeshi, pia ni Mungu wa Yakobo. Kitu kimoja ninachokipenda kuhusu Biblia—kama watu wote ambao Mungu alijishughulisha nao wangekuwa wakamilifu kama Isaya, ningeachwa. Lakini Bwana wa majeshi, pia ni Mungu wa Yakobo—kutenda dhambi…, kujikwaa…, kutenda dhambi kwa kujificha…, hebu nitazame… Yakobo anaweza kuwa mbarikiwa anayepita kwenye bonde la kilio na akamgeukia Bwana na kumuomba nguvu zake.

Niliangalia nyuma miaka mingi Mungu aliyoniongoza. Anajua moyo wangu; anajua kuketi kwangu; anajua kuinuka kwangu; ananijua mimi zaidi kuliko mtu yeyote. Na anajua ninapokuwa mnyonge, ninataka mapenzi yake na ninajua kumpendeza yeye zaidi ya mtu mwingine yeyote. Na vivyo hivyo anajua njia zangu, na ninajua njia zake. Nina furaha kuhubiri Jumapili ya Pasaka hii nikijua kwamba tunamtumikia mkombozi aliyefufuka ambaye ni Bwana wa majeshi, na kwa wale wanaotaka atawale maisha yao; wanaotaka kuyafanya mapenzi yake na wanotaka njia zake; ambao wanyooshao mikono yao juu kwake yeye katika mabonde ya vilio, ninarudia—Hatakuachilia. Nguvu zetu ziko ndani yake kwa sababu yeye yuko ndani yetu.

Yeye ni Bwana wa majeshi, pia ni Mungu wa Yakobo. Anashuka chini akushike mkono wako katika hayo mabonde kama vile baba navyofanya kwa mtoto wake mdogo ambaye bado ana tabia za kitoto. Lakini baba bado atamtafuta.

Bwana wa majeshi anasikia maombi yetu, ni Mungu wa Yakobo. Hauhitaji kuwa Papa ile uweze kumsikia yeye. Jinsi gani ulivyo, katika mazingira yoyote, Mungu—Bwana wa majeshi ni zaidi ya tatizo lako; na kwa sababu yeye ni Mungu wa Yakobo, anapenda kushuka chini, akushike mkono wako, na akuongoze.

Haki© 2007, Mchungaji Melissa Scott. – Haki zote zimehifadhiwa